

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**



TAARIFA KWA UMMA

KERO YA MPAKA KATI YA KENYA NA TANZANIA KUPATIWA UFUMBUZI

Serikali imeahidi kutatua mgogoro wa Mpaka kati ya Tanzania na Kenya katika Kijiji cha Mahandakini, Wilayani Mkinga mkoani Tanga, baada ya kupata malalamiko kutoka kwa wanakijiji wanaoishi katika mwambao huo wa Bahari ya Hindi baada ya kuzuiwa kufanya shughuli zao za uvuvi na kuwasababishia hali ngumu ya maisha.

Hayo yamebainishwa na Naibu Waziri wa Fedha na Mipango Dkt. Ashatu Kijaji, na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dkt. Damas Ndumbaro walipotembelea na kukagua eneo hilo la mpaka na nchi Jirani ya Kenya.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mahandakini, Bw. Nasoro Mbarook, alisema kuwa wavuvi wa Kijiji hicho wanashindwa kuendelea na shughuli za uvuvi baada ya vifaa vyao vya uvuvi kukamatwa na wavuvi takribani 112 kukamatwa na vikosi vya ulinzi vya Serikali ya Kenya nakufunguliwa mashtaka kisha kutozwa faini ya Sh. 5000 ya Kenya, jambo ambalo wavuvi hao wanaamini halikua sahihi kwa kuwa walikua wanavua katika maji ya Tanzania katika Bahari ya Hindi hivyo hawakutenda kosa kama ilivyodaiwa.

Manaiibu Waziri hao, walisema dhumuni la ziara yao katika mpaka huo ni kujionea hali halisi na pia kuweka mikakati ya namna ya kutatua changamoto zilizopo ikiwemo ya wananchi kushindwa kulipa kodi kutokana na kukosa kipato kilichotokana na uvuvi ambapo kwa sasa wanazuiwa kufanya shughuli za uvuvi.

Walisema kuwa wamejionea hali halisi ya mpaka huo hivyo Serikali itafanya tathmini kisha kufanya majadiliano na wenzao wa Kenya ili kulitafutia ufumbuzi suala hilo.

Aidha walibaini kuwa eneo la mpaka halijazingatia taratibu kwa kuwa zipo nyumba ambazo zimejengwa chini ya umbali wa mita 30 mahali ambapo palipaswa kutokuwepo makazi hayo.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Mkinga Bw. Yona Mark, ameiomba Serikali kutoa fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Shule ya Msingi katika Kijiji cha Mandakini Wilayani humo ili wanafunzi waanze kusoma kwa kuwa kwa sasa watoto wanasoma katika shule iliyopo eneo la Kenya.

Pia ameomba kujengwa kwa barabara katika eneo hilo la Kijiji ambalo linawakazi zaidi ya 3666 na Kituo cha kukusanya mapato kwa kuwa eneo hilo kuna bidhaa nyingi zinazoingia na kutoka nchini.

Imetolewa na;

Benny Mwaipaja
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Fedha na Mipango